



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA



Unapojibu tafadhali taja.  
KUMB.MCC/P.10/7/9

14/02/2022

**TANGAZO LA AJIRA YA MUDA, MFUMO WA ANWANI ZA MAKAZI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya MUDA, nafasi 300 kwa mchanganuo ufuatao :-

Nafasi 80 za waandika namba , na wakusanya taarifa 220 kwenye la zoezi la Anwani za makazi katika Kata na Mitaa yote ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

**A.SIFA ZA WAOMBAJI.**

- I. Awe Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-40.
- II. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea wenye taaluma ya TEHAMA, au usomaji wa Ramani watapewa kipaumbele.
- III. Awe anamiliki simu janja yenye teknolojia ya Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima na yenye uwezo Kukusanya majira ya nukta (coordinates) chini ya digrii 4.00 ( kwa wakusanya taarifa).
- IV. Awe na barua pepe (e-mail address) na nywila (password) inayofanya kazi.
- V. Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa, majengo na barabara na kutafsiri ( kwa waandika namba)
- VI. Awe mkazi wa Mtaa husika.

**B. KAZI NA MAJUKUMU**

- a) Kutambua barabara, Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma katika mtaa ( waandika namba).
- b) Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma (wakusanya taarifa)
- c) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, wategemezi, Viwanja, na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa Anuani za Makazi (wakusanya taarifa).
- d) Kutuma data kwenye mfumo wa Anuani za makazi (wakusanya taarifa).

e) Uwezo wa kuchora na kusoma Ramani (wachora Ramani).

**C. MALIPO**

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 30 kwa malipo ya Tshilingi 20,000/= kwa siku.

**D. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;**

1. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Picha (passport size 2)
4. Vyeti vya taaluma.

**E. KAZI INAYOOMBWA**

Kila mwombaji ataje kazi anayoiomba.


**F. JINZI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu, barua pepe na ziwasilishwe kwa watendaji wa kata.

Aidha barua mwombaji ipitie kwa mtendaji wa mtaa husika.

Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe **22/2/2022 saa 9:30 Alasiri**.

Tangazo hili limetolewa na Mkurugenzi wa Jiji.



**TRIPHONIA A. KISIGA**

**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

**MKURUGENZI WA JIJI  
HALMASHAURI YA JIJI  
MBEYA**